(03)

(THE PURPOSE OF LIFE & HUMAN DIGNITY)

MADHUMUNI YA MAISHA NA HESHIMA YA BINADANAMU

Madhumuni,ya maisha ni nini ? Hii ni swali la kawaida ambalo watu wanaliuliza mara nyingi, siyo rahisi kutoa jibu kwa swali hili ambalo linaonekana rahisi lakini ni gumu sana. Ingawa watu fulani wamejaribu kutoa majibu kadhaa kufuatana na jinsi wanavyofikiria, inaelekea kwamba hayo majibu hayawapendezi wasomi. Sababu ni kwamba hawajajifunza kutazama mambo bila kusisimka na kuona vipi kila kimoja kinavyohusiana na kingine. Wameunda taswira akilini mwao kufuatana na kuelewa kwao.Pia tunajua kwamba walimu wengi wa dini, wanafalsafa wakubwa, malenga maarufu na wafikiriaji wakubwa nao hawaridhiki kuhusu maisha. Tunaposoma wanachosema kuhusu maisha inaaelekea kwamba baadhi yao, pia, wanashindwa kupata picha nzuri ya maisha. Wengine wanasema maisha yamejaa mateso, mashaka, na ukosefu wa faraja, wengine wanasema "Ingekuwa vizuri tusingezaliwa kabisa,'' Wengine wanauliza; Kwa nini tumezaliwa katika hii dunia ambayo imejaa mateso?'' Kwa jinsi wanavyoongea tunaweza kuelewa kwamba wameyatazama maisha bila kusisimka, na wameweza kuyaona yalivyo hasa. Lakini watu wa kawaida wanayatazama maisha kijuu juu, yanavyoonekana tu, na sio yalivyo hasa.

Watu wengine wanasema hakuna madhumuni yoyote maalumu ya maisha na kwamba yanaweza kutumika vyovyote vile. Kwa ajili ya nadharia ya namna hii, ni bora tufikirie kwa hekima ili tuweze kuyatumia maisha kwa madhumuni ambayo yana faida kwetu na kwa wengine badala ya kuyapoteza kwa kufanya mambo ambayo sio ya lazima. Kwa njia hii tunaweza kusema madhumuni ya maisha yanategemea jinsi tunavyoyatumia. Tukiyatumia vibaya kwa kukiuka tabia za kiutu, kwa kuiaibisha heshima ya binadamu na kutenda matendo maovu, au kwa kuuendekeza udhaifu wetu wa kibinadamu, haitawezekana kufanya chochote katika maisha. Kwa upande mwingine, ikiwa tutatenda kwa hekima kwa kufuata maadili na kanuni za mbingu na kuwa na subira, uvumilivu, huruma, unyenyekevu na upole, na pia kuwatendea huduma wengine na kuzifundisha akili zetu kuacha upendeleo, basi tutaweza kufanya mambo ambayo ni mema na yenye faida kwa wote Wale wanaokuwa na thawabu hizo watakuwa na amani, furaha, shwari na kutosheka. Maisha yatakuwa na faida kuishi, maisha ya namna hiyo yatakuwa na maana zaidi na yatakuwa na faida kwa kila mtu.

HALI YA MAISHA

" Maisha yanajipoteza yenyewe wakati sisi tunajitayanisha kuishi," anasema msomi mmoja, " Ugonjwa uzee na huzuni ndiyo malipo tunayotoa kwa kuishi katika huu mwili

wetu kama nyumba ,‘’anasema msomi mwingine “Inabidi tulipe gharama ya woga na mashaka kwa ajili ya kuanzisha hamu za kibinafsi’’ haya ni maneno ya mtu wa dini,’ Kuzaliwa kwa mtu ni kuzaliwa kwa huzuni. Kila anavyozidi kuishi muda mrefu, ndio ujinga wake unavyongezeka, kiu yake ya kumudu maisha katika siku zijazo inamfanya ashindwe kuishi sasa hivi,’’anasema mwanafalsafa mwingine wa kichina “Sisi ni matokeo ya tulivyokuwa na tutakuwa matokeo ya tulivyo sasa,’’ anasema Buddha. Tunapoyafikiria haya maoni yote tunaweza kuona na kuelewa hali halisi ya maisha na madhumuni yake. Kama tutakuwa tunazipendeza hisia zetu kama madhumuni ya maisha, basi, lazima tuwe tayari kufikwa na matatizo mengi ambayo yatatokana na kufanya hivyo. Kwa sababu hakuna mtu anaweza kuziendekeza starehe bila kukumbana na matatizo tofauti kutokana na matendo yake. Ingawa wanasayansi wamegundua mambo mengi kumrahisishia kazi binadamu, lakini wameshindwa kuyagundua madhumuni ya maisha, yupo mwanasayansi mmoja anasema “

Kuna madhumuni ya maisha ?
Madhumuni ya maisha ni nini?
Nini,au wapi au lini,
kutoka kwenye anga imekuja mbingu,
limekuja jua, imekuja dunia, yamekuja maisha,
amekuja mwanadamu, na zaidi lazima watafika?
Lakini kuhusu madhumuni, ya nani, au inaelekea wapi?
Kwa nini? Hakuna.

Kuhusu tabia ya mtu, msomi mmoja amesema, “mtu sio kile ambacho yuko hivi sasa, mtu sio kitu asicho hivi sasa,” Kufuatana na maoni yake mtu hafanyi mambo kama mtu hasa. Kufuatana na Ubudha mtu sio kitu ambacho hakibadiliki, ila ni kitu kinachoishi muda mmoja hadi mwingine kufuatana na nishati aliyo nayo. Maisha hayakutokea kwa ajili yupo mtu alikuwa anataka kufanya majaribio kama ya wanyama katika maabara. Maisha ya binadamu yanazo sababu zake yenyewe.

Hatuwezi kuielewa hali halisi ya maisha yetu kwa ajili ya ujinga wetu na uchu mkubwa sana tulio nao. Hii ndio maana tunao uchu wa kuishi ingawa inabidi tunateseka katika dunia hii. Kwa hiyo haiwezekani kwetu kuyaelewa madhumuni ya maisha bila kwanza kuwa na taaswira sahihi

Tunayakataa yale ambayo ni maisha kweli,na tunachagua kile ambacho ni cha muda tu.Hii ndiyo maana tunashinwa kuifikia nirvana;-kwa sababu wakati starehe za maisha yajayo zinawekwa mbele yetu,hatuko tayari kutengana na vitu vya dunia,lakini kama minyoo,tunagaragara kwenye udongo;-na,kwa kifupi,hatuko yayari kutazama juu hata kwa muda mfupi,lakini kama vile tuliyelewa kutokana na kuzumbaa,na usingizi na ulevi,tunapumbazwa na taaswira zetu.

Na kama vile watu wanaotawaliwa na usingizi mtamu wanalala kwenye vitanda vyao sio tu usiku,lakini hata kama asubuhi imefika,na mwangaza wa siku umefika,hawaoni haya kuendelea na starehe,na kuufanya muda wa kazi kuwa wakati wa usingizi na uvivu;-

sisi pia,siku inapokaribia,wakati usiku umekaribia kwisha,wakati wa mchana,tunafanya mambo yale ambayo yanafanywa usiku;kulala,kuota ndoto,kuwa na njozi za anasa;-na macho ya ufahamu wetu yamefungwa pamoja na yale ya mwili wetu,hatuongei kwa usahihi,kila tunachokisema hakieleweki;-hata kama mtu akituumiza jeraha kubwa,akichukua vitu vyetu vyote,akiichoma moto nyumba yetu,wala hatuna habari hata kidogo

Au ni bora zaidi tuseme hatuwasuburi hata wengine kutufanyia hivyo,ila tunajitendea hivyo wenyewe,tunajichoma na kujijeruhi wenyewe.

Unafikiri waovu wenyewe hawawacheki na kuwahukumu wale wenye tabia kama yao?Kwa vile Mungu ameweka ndani mwetu tume ambayo haiwezi kupewa rushwa au kuharibiwa kabisa,hata tukishuka katika uovu kiasi gani;-kwa hiyo hata waovu wanajihikumu wenyewe,na ukiwaita vile walivyo,wanaona haya,wanakasirika,wanasema kwamba hiyo ni matusi Kwa hiyo wanahukumu wanachofanya ,hata kama siyo kwa matendo yao,lakini kwa maneno yao,akili yao inawalaumu,hapana,hata kwa matendo yao.Kwa sababu wanapofanya vitendo vyao mafichoni,ili wasionekane,wanatoa ushahidi mkubwa kuliko wote juu ya maoni waliyo nayo kuhusu jambo lenyewe.Kwa sababu uovu ni dhahiri sana kiasi kwamba watu wote wanaulaumu,hata wale ambao wanaufuata;-na thawabu,inapendwa hata na wale wasiokuwa nayo.Kwa sababu hata mzinzi anausifu useja,mtu anayetamani vitu vya wengine,anaisifu haki,mtu mwenye jazba anaisifu subira,na kuilaumu tabia ya mikwaruzano na ugomvi,na malaya anaulaumu umalaya.

Vipi sasa(unasema)anavifuata hivi vitu?Kwa ajili ya uvivu kupita kiasi,sio kwa sababu anafikiria ni jambo jema;ama sivyo asingelionea haya jambo hilo,au kulikana wengine wanapomshutumu.Sio hivyo tu ,wengi,kwa kushindwa kuvumilia aibu,wamejinyoga waliposhutumiwa kwa uovu wao..Kwa sababu akili yao wenyewe inawalaumu.Kwa hiyo mambo mema yanang'ara kama jua.Kinyume chake,mambo ya ovyo ni chukizo.

NISHATI KATIKA VITENDO.

Maisha yameekezwa kuwa ni muungano wa akili na vitu. Kutokana na muungano kiumbe kinatokea na kinaendelea kuishi mpaka msambaratiko unapotokea. Lakini nishati ya akili na vitu vilivyosambaratika vinajikusanya tena katika miundo tofauti, katika dunia tofauti, na mtu anaishi kama alivyokuwa katika maisha yake yaliyopita. Hii inaendelea tena na tena iwapo nishati katika vitendo na uchu wa kuishi unabakia.

KANDA TANO.

Neno kanda linatumika, kama tunavyosema, ' kanda ya kaskazini,'' kanda ya kusini,' Kufuatana na Ubudha, mwili wa binadamu unazo kanda tano; kanda ya umbo, [rupa], kanda ya hisia, vedana, hisia maana yake kuwa na furaha au kuwa na maumivu; kanda ya hisi, sanna, perception, maana yake ni zile hisia zinazotumika katika vitendo; kuzungumza, kutembea, kushika vitu kwa

mikono,uzazi, kutoa uchafu ndani ya mwili,kanda ya mawazo, sankhara, ni mawazo yoyote mtu aliyo naye ambayo ndio msingi wa maadili, au msingi wa utendaji mzuri wa akili, kanda ya ufahamu, vinnana, consciousness; uwezo wa kuwa macho, nazo ni aina tatu, kuwa macho(waking consciousness), kusinzia(deep sleep conciousness), kuota ndoto(dream consciousness). Zipo aina nne za vitu; vitu vigumu, maji, moto, hewa. Vitu vigumu pamoja na vinne vya akili yaani vedana, sanna, sankhara na vinnana ndio vinaunda mwili.

Uchambuzi huu wa maisha ulitoa changamoto kubwa sana kwa imani nyingi za kidini wakati fulani kwa sababu, kufuatana na Budha hakuna kitu chochote kinachoweza kuitwa maisha ambayo yanadumu milele, bila kubadilika, bila kumong'onyoka.
Mwili sio kitu chochote isipokuwa tu ni mkusanyiko wa kemikali ambazo zinabadilika kila wakati. Maisha ni tone katika mto unaokwenda mbele daima.

DUNIA NI MKUSANYIKO WA MAWIMBI;

Uchambuzi wa kisayansi wa mbingu unaonyesha kwamba dunia siyo kitu chochote ila mkusanyiko wa mawimbi. Dr, Einstein alisema, "Vitu vyote vimeundwa kwa mawimbi, na tunaishi katika dunia ya mawimbi" yapo mawimbi ya mwangaza, mawimbi ya sauti, vitu vingine vinatambuliwa kwa kunuswa, au kutambuliwa na ulimi, au kwa kuguswa na mkono, lakini vyote ni mawimbi.
"sisi wote ni sehemu ya mawimbi yale yale,
kama mtu anaweza kuelewa
juu ya hali ya mwili wake
na hisia zake,
juu ya akili yake na
vitu ambavyo vimo katika akili yake.
Kuelewa huku kutamsaidia kufahamu kama yapo madhumuni yoyote katika maisha.

JIBADILI.

Unaweza kupata nini kwa kuibadili dunia? Unaweza kupata ukamilisho? Haiwezekani.; Ni majivuno yako tu ndio yatakayoongezeka. Utakuwa bado umekwama katika gurudumu la maisha. Lakini kwa kujibadili, kwa kuielewa hali ya nafsi yako , kwa kujitolea mhanga, kwa kuwa na nidhamu, na kwa juhudi, utakamilika. Ukikamilika, maisha yako yatakuwa na maana zaidi na unaweza kuwafanyia msaada mkubwa watu wengine. Watu watauiga mfano wako, watakufuata wewe, na pia watalifikia. Lengo lao la maisha.

Binadamu leo ni matokeo ya mamilioni ya mawazo yake na matendo yake ya zamani. Haji amekwishatengenezwa tayari , anaumbwa na anaendelea kuumbwa. Tabia yake inatokana na jinsi anavyofikiri, mtu kwa asili yake sio mkamilifu, inabidi ajifunze kukamilika. Sio binadamu tu ndiyo wenye maisha katika hii mbingu. Hata hivyo binadamu wana uwezo mkubwa zaidi wa kufikiri na wa mantiki. Kwa ajili hiyo binadamu ni bora kuliko viumbe wengine kwa sababu anao uwezo wa kuyatengeneza maisha yake ili aweze kuyaondoa mateso ya dunia. Kwa hiyo, kama madhumuni ya

kuishi ni kuondoa tu mateso, basi wanadamu wanaweza kufanya hivyo kwa juhudi zao wenyewe, lakini maisha yatakuwa ni hasara yasipotumiwa vizuri.

Buddha katika mafundisho yake anatilia mkazo faida ya kuwa binadamu. Alichora picha kamilifu kabisa ya binadamu anavyojitahidi na kung'ang'ania maisha baada ya maisha katika lengo lake kufikia ukamilifu. Maisha ni kitu cha kipekee. Hayawezi kulinganishwa na kitu chochote," thamani yake haiwezi kupimwa kwa kulinganishwa na vitu vingine, na fedha haiwezi kuyanunua, Lakini, licha ya kuwa na tunu kama hii wengi hawajifunzi jinsi ya kuitumia. Hapa maisha maana yake sio tu mwili au hisia, ila akili ya binadamu inayofikiri.

JINSI YA KUWAPANGA WATU

Budha aliwapanga watu katika makundi;

1, Yule anayefanya kazi kwa faida yake, lakini sio kwa faida ya wengine.
2. Yule anayefanya kazi kwa faida ya wengine,na sio kwa faida yake.
3. Yule ambaye anafanya kazi sio kwa faida yake au ya mwingine. ,
4. Yule ambaye anayefanya kazi faida yake na kwa faida ya wengine.

Yule anayefanya kazi kwa faida yake, na sio kwa faida ya wengine., huyu ndiye anafanya bidii kuyaondoa kabisa mawazo mawazo maovu, maneno maovu na matendo maovu aliyonayo, lakini hawawashawishi wengine kuondoa tamaa, chuki na ujinga.

Mtu anayefanya kazi kwa faida ya wengine na sio kwa faida yake., ndiye yule anayewaambia wengine waache vitendo viovu, na maneno maovu, lakini yeye hafanyi bidii kuondoa tamaa, chuki na kuzubaa. Yule ambaye anafanya kazi sio kwa faida yake au kwa faida ya wengine. Ndiye yule ambaye yeye hafanyi juhudi kuondoa uchu, chuki,na ujinga, na pia hawashajiishi wengine kuacha uchu, chuki na ujinga.

Yule anayefanya kazi kwa faida yake na ya wengine , ni yule ambaye anafanya juhudi kuyaondoa mawazo, maneno na matendo maovu aliyonayo, na pia anawashajiisha wengine kuondoa uchu, chuki, na ujinga.

MAISHA YANAWEZA KUWA NA MATESO

Tukifikiria sana tunaona kwamba kuna mateso mengi katika maisha, kila wakati tunateseka. Katika mwili, katika hisia, katika akili. Yupo mtu yeyote katika dunia hii ambaye hana maumivu ya mwili, hisia au akili? Hata wale ambao wamefikia utakatifu hawako huru kutokana na mateso ya mwili, wakati miili yao bado inadumu. Maisha na mateso hayawezi kutenganishwa.

Mtu yoyote akiuliza "Ni kitu gani ambacho kuliko vyote hakina uhakika katika dunia hii?" Jibu sahihi litakuwa, maisha ni kitu ambacho hakina uhakika , kila kitu tunachofanya katika dunia ni kukwepa au kuepuka mateso au kifo, tukiyapuuzia maisha yetu kwa nukta moja tu, hiyo inatosha kupoteza maisha yetu, utaratibu wetu wa kila siku, kama vile kufanya kazi, kula, kunywa, kulala, na

kutembea ni njia tunazotumia kukwepa mateso na kifo. Ingawa wakati mwingine tunaweza kustarehe kidogo kwa kutimiza haja fulani, lakini muda unaofuatia kile kile kilichotuletea starehe kinaweza kukubalika kuwa mateso. Kwa hiyo, hazina bora ya amani na furaha sio lazima iwe katika nyumba ya mtu tajiri, inaweza kuwepo katika nyumba ya mtu aliyeziacha starehe za dunia.

Kila kitu katika maisha yetu kinaathiriwa na kubadilika na kutotosheleza. Ndio maana Budha alisema kwamba uchu wa starehe za dunia ukibakia, au hamu ya kuishi ikibakia, hakuna njia yeyote ambayo unaweza kuyaepuka mateso. Hamu ni muhimu ili uweze kuishi. Maisha yakiwepo mateso hayawezi kuepukika.

Wengi wanawaza jinsi ya kuishi maisha milele, lakini, la kushangaza, watu wengi wanaotaka kuishi muda mrefu wanaona maisha yanachosha, kiasi kwamba hata muda wa siku moja hawajui waishi vipi. Kuna methali ya kichina kuhusu tamaa ya mtu kutaka kuishi muda mrefu, “Binadamu anajidanganya., anasali ili aweze kuishi maisha marefu, lakini anaogopa kuzeeka.” Labda anachotaka ni kubakia kijana milele ili aweze kufaidi starehe za dunia. Budha anasema hii hamu ya kutaka kuishi milele ni chanzo kimojawapo cha hamu za ubinafsi na mateso

Ni rahisi kuwa mchangamfu
Wakati maisha yanapokwenda kama wimbo,
Lakini mtu wa maana,
Ni yule anayeweza kutabasamu, maisha yanapokwenda vibaya.
Kila furaha kidogo tunayoipata, inakuja baada ya kushindwa mara nyingi. Mtu hawezi kupata maisha pahali ambapo hakuna ugumu, matatizo, migongano, na maelfu ya masumbufu. Usiku na mchana binadamu anajitahidi kuziondoa hizi hali ambazo hazifai. Kila anapozidi kujikwamua kutoka kwenye tatizo moja ndivyo anavyozidi kukabiliwa na lingine linalotokea. Anapofaulu kuliondoa tatizo moja, basi kwa kukusudia au bila kukusudia, anatengeneza matatizo mengine. Mwisho wa matazo haya uko wapi? Ili tuweze kuishi, inabidi tuyapokee mateso haya bila manung’uniko. Hakuna njia nyingine. Mateso yatakuwepo siko zote. Lakini mateso na huzuni sio lazima yawepo, Budha anasema, ‘mateso ni ugonjwa ambao unaweza kutibiwa kikamilifu wakati utakaso au ukamilisho unapopatikana.

Lao_Tze, mwalimu wa kichina anayefahamika sana amesema, ‘Nimeteseka kwa sababu nina mwili, ningekuwa sina mwili ningeteseka vipi?
“Kama milima yote ingekuwa vitabu na kama mito yote ingekuwa wino na kama miti yote ingekuwa kalamu, bado isingetosha kuieleza huzuni yote ya dunia hii. {Jacob Boehme}.

Unapotazama watu wanavyoteseka katika dunia hii, ndipo unapoweza kuielewa hali halisi ya dunia hii. Kwa nini wanateseka namna hii? Na ni nani anayesababisha mateso yao? Budha anasema kila mtu anayasababisha ,mateso yake mwenyewe. Wanateseka hapo leo kwa sababu ya uchu mkubwa walio nao wa kutaka kuishi, kwa sababu huo uchu mkubwa unasababisha watende matendo maovu, Hii ndiyo sababu kuu ya mateso .Imechukua zaidi ya miaka 2500 kwa wanafalsafa wengi na

saikolojisti wengi kuelewa kwamba alilosema Budha ni kweli. Mshairi mmoja aliyaelezea maisha yetu kwa njia hii.

“Mdudu anakimbilia moto
Hajui kwamba atakufa
Samaki wadogo wanaitafuna ndoano,
Hawajui hatari yake,
Lakini fikra inafahamu fika hatari iliyopo,
Katika hizi starehe za kiovu za dunia,
Bado tunazing’ang’ania kwa nguvu,
Ujinga wetu ni mkubwa sana.

MAISHA HAYADUMU

Ubudha unafundisha kwamba muda wa maisha ni mfupi sana kwa hiyo inabidi tufanye kazi kwa bidii, na kwa uangalifu ili tupate uokovu wetu.
‘watu hawawezi vizuri mpaka tuelewe
Kwamba tupo hapa kwa muda mfupi
Lakini wale wanaouelewa ukweli huu,
Wanaepuka mateso na kugombana .
{Theragatha}

DUNIA UWANJA WA MAPAMBANO

Mbingu yote ni uwanja mkubwa wa mapambano. Maisha sio kitu chochote kile isipokuwa ni mapambano yasiyokwisha. Akilini ndipo kuna mapambano makubwa kabisa. Mtu ambaye hana amani yeye mwenyewe katika nafsi yake, hawezi kuwa na amani na dunia, na vita vya nje, inabidi ziendelee ili kuuficha ukweli kutoka kwa watu kwamba vita kweli ipo ndani. Sala ya maana kuliko zote leo ni sala ya amani, furaha, na fanaka, Lakini haiwezi kuwepo amani katika hii dunia iliyojaa vita mpaka migogoro iliyopo ndani ya akili ya binadamu iishe.

Machoni kwake Budha, viumbe wote wanatetemeka kama samaki waliomo kwenye mfereji ambao umekaribia kukauka, walivyoshikwa na uchu, wanaruka huku na huku kama sungura aliyenaswa kwenye mtego au mishale ilyopotea ilyorushwa usiku, Aliuona ugomvi wa wote dhidi ya wote, aliuona ugomvi usio na maana wa wanyama kama simba au chui au wale ambao wanawavizia na kuwadhulumu wanyama wengine maisha yao, baadaye na wao wanatafunwa. Vita inasababishwa na akili ya binadamu na binadamu huyo huyo anaweza kuleta amani na hak iakiitumia akili bila ubaguzi.

Historia ya dunia, ubaguzi wa rangi, ugaidi wa kidini na tamaa ya nguvu za kisiasa au tamaa ya utajiri vimeleta maafa makubwa, huzuni na mateso katika dunia hii. Imesababisha wengi sana kupoteza maisha yao kwa njia kikatili. Mambo kama haya hayajasaidia hata mara moja kuleta fanaka na maendeeleo ya dunia. Watu wenye kiu ya kupata cheo au fedha na wamelewa husuda siku zote

wanaleta matatizo na mara nyingi wanajaribu kuhalalisha matendo yao ya kikatili katika jina la amani na haki. Tunaishi katika dunia ambayo watu wanajidanganya. Inaonekana kuna umoja, lakini kimawazo, watu wamegawanyika. Wakati mwingine, upo muungano wa mawazo, lakini watu wanaishi mbali mbali, mmoja mashariki, mwingine mashariki ya kati. Msemo unaofuata unaonyesha jinsi mabadiliko yanavyotokea katika maisha yetu.

"Tunaishi na kufanya kazi na kuota,
Kila mtu anayo agenda yake ,
Wakati mwingine tunacheka,
Wakati mwingine tunalia,
Na hivyo ndivyo siku zinavyokwenda

UPUUZI MWINGI.

Matizo mengi machozi mengi
Watu wengi fedha nyingi
Muda mwingi Na yote kwa nini?
Matatizo mengi kwaajili ya mwili mdogo

Rundo la preoini
Linalokunjuka upesi
Maiti ndogo
Inaoza upesi
Haiitwi tena
Baba mpendwa, mama
Au mpendwa yoyote
Licha ya hivi
Lazima tuwe
Na faraja ya majeneza
Maandamano na jiwe la laburi
Mikusanyiko na maombolezo
Misa na ibada.
Amezikwa au kuchomwa moto,
Au kuhifdhziwa milele na kemikali
Yote kwa ajili ya
Hii miili iliyofumuka,
Vijana kumbukeni
Wajukuu wadogo
Na baada yao,
Waliokufa wanasahauliwa.
Kwa hiyo huu sio upuuzi mtupu? {Bhikkhu Khantipale}

THAWABU ZA KIROHO

Julian Huxley anasema, maisha lazima yafungue milango na kumwezesha mtu kupata maendeleo ya mwili, akili na roho_ chochote kile ambacho binadamu anaweza kukifanya. Na binadamu anaweza kufanya mambo ambayo nini makubwa zaidi, au ya maana zaidi.

Unazaliwa katika dunia hii kufanya wema fulani na sio kupoteza muda wako katika uvivu. Ukiwa mvivu, unakuwa mzigo katika dunia hii. Kila wakati fikiria jinsi ya kupanda juu zaidi katika wema na hekima. Utakuwa hauitumii vizuri bahati yako ya kuwa mwanadamu usipoonyesha kwamba umestahili kuletwa hapa. Kupoteza muda wako kwa kuhuzunika kuhusu mambo yaliyotokea zamani, au katika uvivu, au katika kufanya mambo bila uangalifu itaonyesha kwamba hustahili kuwepo katika dunia hii.

Mti wa ustaarabu(civilization)unayo mizizi yake katika thawabu za kiroho,hili ni jambo ambalo wengi wetu hawajalielewa Bila mizizi hii majani yake yote yatanyauka,na kitabakia kisiki kisichokua na maisha.

Budha alitushauri tuache uvivu,tuinuke tufanye kazi,na tujaribu kupata fedha ,tutunze tulicho nacho na tusiwe wabadhirifu .Budha aliyatazama maisha ya dunia kwa usahihi,kwa kuangalia kila kitu kinahusiana vipi na kitu kingine,bila ubinafsi au dharau.Kwa upande mwingine,walimu wengine wa dini wamesema tukiyaachia maisha haya yazunguke tena na tena katika mzunguko wa maisha na kifo,huku tukiteseka kimwili na kiroho,basi kutakuwa hakuna madhumuni yoyote katika maisha haya. Lakini tunaweza kuyatumia maisha haya kwa madhumuni yanayofaa zaidi iwapo tutawasaidia wengine kwa kuendeleza maadili,kwa kuizoeza akili,kutafakari na kuishi kama watu wastaarabu kwa amani na muafaka na dunia yote .Budha amesema binadamu siyo kalagosi ambao hawana majukumu. Binadamu ni kiumbe aliyeendelea kuliko viumbe wote.Falsafa ya zamani inayaeleza maisha kwa njia hii"Kutoka kwenye giza kwenda kwenye mwangaza,kutoka kwenye uongo kwenda kwenye ukweli,kutoka kwenye mauti kwenda kwenye uhai"

KUISHI BAADA YA KIFO

Maswali yote anayouliza binadamu yanahusu uhakika wa kifo.Binadamu inaelekea nai tofauti na viumbe wengine .Binadamu hataki kuambiwa kwamba inambidi kufa kama viumbe wengine.Kama mtu angejua tu kwamba maisha ni mafupi na kufa ni lazima,angeweza kuyatazama matatizo mengi yanayohusiana na maisha.Katika kukipinga kifo,mtu amfeanikiwa kuyarefusha maisha yake,ambayo inaweza kufananishwa na mtoto anayecheza na nyumba ya mchanga aliyoijenga ufukoni mwa bahari kabla haijapigwa na wimbi lingine.Mtu mara nyingi amefanya kifo kuwa ndiyo kiini cha shughuli za kidini,na ameomba baraka za mbinguni ili aweze kuishi milele.

Kifo ni kitu cha uhakika kwa viumbe wote,lakini ni mtu peke yake ,kutokana na uoga wake wa tishio la kifo,ndiye ameunda dhamira ya kudumu.Na katika hiyo hamu ya kuendelea kuishi kwa njia moja au nyingine,binadamu ameunda dini,nayo dini injaribu kumpa mwisho wenye maana zaidi kwa maisha yake .

Ingawa dini nyigine zinaamini kwamba yapo makazi ya mbinguni ambapo maisha ni raha isiyokwisha,bado hatujasikia kuhusu wafuasi wakereketwa wa dini yoyote ambao wamekuwa tayari kuacha maisha yao ya duniani na kwenda kuishi na Mwenyezi Mungu. Hata Wabudha wanapendelea zaidi kuyang'ang'ania maisha yao ya thamani ya duniani ingawa wanafahamu fika kwamba ni mateso tu,na kwamba furaha ya mwisho ipo katika wokovu kutokana na mateso.

Tatizo moja kubwa linalozikakabili nchi nyingi duniana ni mlipuko wa watu. Nji na mbinu lazima zitafutwe kulithibiti ongezeko hili la maisha lisilokwisha.Hawa mamilioni wanahitaji chakula,makazi,starehe na usalama.Kwa watu hawa swali siyo ,'Madhumuni ya maisha',ila,'Tuyafanye nini maisha'' Jibu rahisi kwa swali hili lingekuwa ni bora tuyatumie maisha kwa kadiri tunavyoweza na rasilimali zote,na tutafute furaha yoyote ambayo tunaweza kuipata kihalali badala ya kuwa na wasiwasi kupita kiasi kuhusu madhumuni ya maisha au kuanza kufikiria hoja kwamba maisha yana madhumuni ya kiroho.Lakini dini inaingia kati kumfariji binadamu,au kumwamsha aelewe kwamba maisha siyo kitu cha uchovu au kisichokuwa na matumaini,kama kinavyotazamwa mara nyingi katika dunia hii tunayoishi. Yapo matumaini ya maisha mazuri zaidi.

Maendeleo yaliyoletwa na binadamu katika maisha haya inatokana na kwamba anatambua kwamba anadumu milele na kwamba angependa kuacha alama yake nyuma baada ya kuondoka.Kama mtu angekuwa na uwezo wa kuishi milele juhudi yake ya kazi ingepungua,angekuwa hana motisha ya maendeleo,angekuwa hana hamu ya kuifanya dunia kuwa nzuri zaidi ya jinsi alivyoikuta.Kungekuwa hakuna kifo,maisha yangechosha sana,yangemelmea mtu .Kama mtu angeweza kufahamu atakufa lini,lazima angefanya mambo tofauti na jinsi anavyofanya sasa.

' Mwili wa mtu unabadilika kuwa vumbi,lakini taathira yake inaendelea' amesema .Budha .
Ingawa waliotangulia wamekufa na hawapo ,tunaweza kusema kwamba bado wapo mingoni mwa wengine. Tunaweza kusema kwamba ingawa hawapo kimwili ,lakini taathira yao bado ipo.Tunaposema waliotutangulia hatumaanishi tu babu zetu,ila wale waliochangia katika faida,furaha na fanaka ya dunia. Kwa maana hii tunaweza kusema kwamba mashujaa,wahenga ,malenga na wanafalsafa wa zamani bado wanaishi mingoni mwetu.Tunaweza kusema kwamba tunakula nao sahani moja,mawazo yao ya hekima na malengo yao matukufu,hata pia muziki mzuri wa karne nyingi.

Kilio cha ndani ya moyo wa binadamu kutafuta madhumuni ya maisha kunaonyesha kwamba binadamu anatambua kidogo hali ya maisha .Mtu akielewa kwamba anayo roho.hatalilia madhumuni ya maisha,kwa sababu ataelewa kwamba yeye ndiye madhumuni.

Watu wafikiriaji wametambua kwamba historia ya umma wa binadamu haiamuliwi na mambo yanayotokea angani,ila na yale yanayotokea katika mioyo ya watu.

Mtu anaweza kujiinua,na ni lazima ajiinue juu ya upungufu wowote uliopo katika nafsi yake,lakini hapaswi kujiinua juu ya sheria Wakristu,kwa mfano,wanafahamu kwamba Herod alipokuwa akiongea mbele ya umati wa watu,wale watu walianza kupiga kelele,'Ni sauti ya mungu,sio sauti ya mtu',tumbo lake Herod lilipasuka pale pale ,utmbo ukatoka nje,akafa.

YATUMIE MAISHA VIZURI

Jambo muhimu kuhusu maisha ni kwamba tunayo na ni lazima tuyatumie vyema kadiri tunavyoweza.Hii ndiyo faida kubwa ya maisha,ile fursa tuliyo nayo ya kuyatumia vizuri kwa kadiri ya uwezo wetu.Watu wengi wanaishi maisha ya huzuni kwa sababu hawataki kuyatumia maisha ipasavyo,muda mwingi wanaishi kwa mashaka,wanafanya kazi ili tu waweze kuyamudu maisha,wanafanya kazi kama watumwa ,wanakabiliana na matatizo makubwa na vikwazo.Tunatumia nguvu zaidi katika uwanja wa vita-tunapigana ili tuweze kuwa hai,tunapigana ili tupate vyeo,tunapigana ili tupate utajiri,tunapigana ili tupate jina,tunapigana ili tupate starehe na tunapigana ili tujiepushe na hatari.Wakati mwingine tunapata furaha kidogo,lakini kila furaha mwisho wake inakuwa mateso.

Itazame dunia na utaona jinsi watu wanavyopigana;wanalipua mabomu,wanafanya utekaji nyara,na wanaleteana madhara.Dunia nzima ni kama nyumba ya vichaa.Watu wamazisahau tabia zao nzuri za kibinadamu,na wameruhusu ufisadi,ukatili,dhuluma.unyang'anyi,kuweka hasira moyoni,kisasi,tamaa na ujinga viwatawale.Inaelekea hakuna nafasi katika akili ya binadamu ya kupandikiza mawazo mazuri.Katika hali hiyo,mtu anaweza vipi kupata amani,furaha na fanaka,katika uwanja wa vita ambapo watu daima wanapigana,kwa ajili ya kupata fedha au kwa ajili ya kuepuka hatari?Ukatili wa binadamu kwa binadamu mwenzake unayafanya maelfu yasiyo na hesabu kuomboleza.

Ukiielewa hali halisi ya dunia na maisha,basi unaweza kuelewa mara moja kwa nini ni muhimu kabisa upate wokovu.-nirvana-na hautachelewa katika juhudi zako za kuitafuta hii hali ya furaha. Leo unajitahidi kuyaepuka mateso yako kwa njia ya kidunia,vita hiyo lazima utashindwa.Lakini ukijaribu kuyaondoa mateso yako kwa kuiendeleza roho yako,hapo utapata amani,na furaha na fanaka.Hiyo ni nirvana.

FURAHA ZA DUNIA

Tunafahamu kwamba wapo wengi katika dunia hii,hata miongoni mwa Wabudha,ambao hawako tayari kufanya kazi ili wapate nirvana. Kwa ajili hiyo,wengine wameanzisha tafsiri yao wenyewe ya nirvana kama paradiso ambapo watu wanastarehe milele kataka starehe za hisi.Tafsiri kama hii itawapendeza wale ambao wana uchu mkubwa sana,na ambao wanayang'anga'nia sana maisha yao na starehe za dunia. Hawawezi kuelewa kwamba tafsiri hiyo ya nirvana ni ndoto tu. Hata hivyo, wanaifikiria na kusali ili wapate nirvana ya aina hii. Kwa upande mwingine,kuna watu wengine wanaofikiria kwamba ni bora kubakia katika dunia hii ingawa kuna mateso sana,,waweze kufaidi maisha yao.Wanashindwa kuelewa kwamba kwa ajili ya uchu walio nao na tamaa walizo nazo,hawawezi kutambua kwamba furaha ya nirvana ndiyo pekee furaha ya milele,na ile

furaha nyingine ya kidunia ambayo wanayoidhania ni furaha haiwezi kuyaondoa mateso yao ya mwili au akili.

Budha amesema,ni kwa ajili ya ujinga ndio watu wanakuwa na uchu wa kuishi katika maisha haya ndani ya hii samsara,mzunguko wa maisha na kifo,huku tukivumilia mateso na kuvikimbilia vitu ambavyo havifikiki katika kutafuta kitu cha kuzifurahisha hisi zetu.Lazima tujifunze kuzifanya hisi zetu ziwe shwari badala ya kuziendekeza kwa kuzipa starehe ambazo hazidumu.

MUUNDO WA DUNIA USIOKWISHA

Watu wengine wanafikiria kwamba kama wote tukipata nirvana,hii dunia itakuwa tupu na kwamba hakutakuwepo mtu yeyote kufanya kazi kwa maendeleo ya dunia.Hili siyo wazo sahihi linalitokea katika mawazo ya watu hawa ambao hawana elimu sahihi ya viumbe.

Lazima waelewe kwamba hii dunia haiwezi kuwa tupu kwa sabau ni watu wachache tu wenye hekima watakaoweza kuifikia nirvana.Kuhusu miundo ya dunia,haina kikomo.Na hakuna mwanzo au mwisho wa mbingu.Mbingu daima itatokea na kutoweka .Muundo mmoja wa dunia ukitoweka,mwingine unazaliwa .Muundo wa dunia uliosambaratika na viumbe vyake,vinakuja pamoja tena,mtu asifikirie kwamba ipo idadi kamili ya viumbe ambao wanatokea na kutoweka. Idadi ya viumbe inaongezeka bila kikomo.

MAENDELEO NA UHARIBIFU WA MAZINGARA

Tunafanya kazi kweli hapa kwa ajili ya maendeleo ya dunia?Tunaweza kufikiria ndivyo tunavyofanya,lakini hasa tunaiharibu dunia.Tumegundua vitu vingi vya kuiteketeza dunia.Maumbile yanatupa vitu vingi katika dunia hii Kufikia malengo yetu,tunaharibu uzuri wa dunia.Tunaichafua anga,maji na hewa.Tunateketeza mimea na wanyama.Tusifikirie kwamba kwa vile sisi ni binadamu,basi viumbe wengine hawana haki ya kuishi katika dunia hii. Kila kiumbe kingine kina haki sawa ya kuishi hapa.Tusiwanyime viumbe wengine haki zao.Sio hivyo tu,katika jamii ya binadamu,rangi moja inajitahidi kuiangusha rangi nyingine,kuzuia maendeleo yao ,kuleta vizuizi ili wasiishi kwa amani. Wanaanzisha vita na kuchinjana yote katika jina la uzalendo na uzawa.

Kama binadamu wanazo akili zilizochafuka.kutakuwa hakuna amani na fanaka duniani.Ni kwa ajili ya kuwepo kwa watu kama hao,ndiyo hii dunia imekuwa pahali pa vurugu.Leo tunaona umwagaji mkubwa wa damu duniani kote.Kila mmoja wetu anafanya mpango wa kumtapeli mwenzake.Mawazo ya ubinafsi yamejaa akilini mwao.Mtu mmoja hawezi kumwamini mtu mwingine. Mtu mmoja hawezi kuielewa hasa tabia au nia ya mtu mwingine

MTU NDIYE ANAYEHUSIKA

Watu daima wanaongea kuhusu kutokuwepo kwa uhakika katika hali ya dunia.Nani ameisababisha hali hii mbaya?Ni yeyote yule zaidi ya mtu anayedaiwa kuwa mjanja

sana?Tunaweza kutegemea dunia bora ya a amani,furaha na fanaka ikiwa watu wanazo tabia ambazo siyo za kistaarabu?Tunaweza vipi kuyafaidi maisha yetu katika dunia hii ambayo haina uhakika?Wanasayansi wanataka kuyashinda maisha kwa sababu zao wenyewe za kidunia.Dini na falsafa zinataka kuishi kwa mahusiano mazuri na maumbile ili kupata amani ya akili. Na maendeleo ya kiroho.Huwezi kuibadili hali ya dunia upendavyo;lakini unaweza kuyabadili mawazo yako ili uwe na roho ya kutosheka,jambo ambalo linaweza kukuletea furaha. Mtu ambaye anang;ang;ania tu kuzipata starehe za dunia hawezi kuifikia elimu ya juu,kwa sababu haipatikani bila kuitafuta kwa bidii. Maendeleo ya vitu yanamfanya mtu anakuwa kama mnyama,lakini maendeleo ya kiroho yanamuinua mtu.Katika maisha ambayo watu wanatafuta tu maendeleo ya vitu,watu wanakuwa watumwa wa hisi zao.Ni kawaida,watu wengi hawataki kuukabili ukweli wa maisha.Wanapenda kujiliwaza kwa kujiona wako salama,kumbe hawako salama,na kuota ndoto nzuri,na kutaswiri mambo mengine,na kufikiria kwamba kivuli ndiyo kitu chenyewe .Msimamo wa Budha kuhusu vyeo na starehe za dunia ni,"Bora kuliko kutawala dunia,bora kuliko kwenda mbinguni,bora pia kuliko kuwa mtawala wa sayari kadhaa,ni kuifikia ngazi ya kwanza ya mwanafunzi-ngazi ya kwanza ya ukamilisho."

Kwa kuyatumia maisha yake kwa maendeleo ya vitu ya dunia ili ailishe hamu yake ambayo haishibi haiwezekani mtu kuuona mwisho wa matatizo yake katika dunia hii.Budha anasema dunia hii imejaa kupingana kwingi;anasema tena,njia ya kuzipata faida za dunia ni moja;-na njia inayoelekea kwenye nirvana ni nyingine.

MTU NA ASALI YAKE

Hapa ipo hadithi kutusaidia kuelewa hali hasa ya maisha na starehe za dunia.Mtu alipotea njia alipokuwa akipita kwenye msitu mkubwa uliojaa miba na majabali.Halafu akakumbana na tembo mkubwa aliyeanza kumfukuza. Akakimbia kuyaokoa maisha yake.Alipokuwa anakimbia akakiona kisima na akafikiri kwamba hiyo ni sehemu nzuri ya kumtoroka tembo aliyeanza kumfukuza. Lakini kwa bahati mbaya akamuona nyoka mkubwa chini ya kisima.Lakini kwa vile hapakuwepo mahali pengine pa kukimbilia kumtoroka yule tembo,akaingia katika hicho kisima na akafaulu kuushikilia mmea unaotambaa uliokuwa umeota kwenye ukuta wa hicho kisima.Alipokuwa amejishikilia kwenye huo mmea aliwaona panya wawili,mmoja mweupe,mmoja mweusi Alistuka kuona kwamba kuwa wale panya wawili walianza polepole kuutafuna ule mmea,ambao ndio ulikuwa kama ndio kamba aliyokuwa ameishikilia Lakini hapo karibu akauona mzinga wa nyuki,ambao ulikuwa unatoa matone ya asli.

Akikabiliwa na kifo chake kwa njia tatu tofauti katika ile sehemu ya hatari aliyokuwepo,akaanza kuila ile asli kwa uroho.Halafu mtu akapita na alipoiona ile hali yake huyu mtu maskini ya kusikitisha ,akajitolea kumpa mkono ili ayaokoe maisha yake.Lakini mtu huyu mroho na mjinga hakutaka kumsikiliza kwa ajili ya utamu wa asali.Utamu wa asali ulikuwa umemlewesha kiasi kwamba aliamua kuipuuzia hatari iliyokuwa inamkabili..

Hapa katika hii hadithi,njia yenye miiba ya msituni inafananishwa na samsara,gurudumu la maisha Tembo hapa maana yake kifo. Kifo daima kinatufuata na kutufanya daima tusiwe na furaha na kutufanya tusijione salama akilini.Mmea unaotambaa ni kuzaliwa kwetu.Kama vile mmea unaotambaa unavyozidi kukua na kujivingirisha kwenye mimea mingine,hivyo hivyo kuzaliwa kwetu kunazidi

kuongezeka,kushikilia na kung'ang'ania vitu vingi visivyokuwa vya lazima katika dunia hii.Wale panya wawili,mweupe na mweusi,ni usiku na mchana,Tokea siku tunayozaliwa,usiku na mchana unafupisha maisha yetu. Matone ya asali ni starehe za dunia ambazo hazidumu,na ambazo zinazmshawishi mtu abaki katika hii dunia ambayo haidumu na haina uhakika.Yule mtu mpole aliyetoa mkono wake kusaidia ni nani?Yule ni Budha aliyetaka kumuokoa mtu kutokana na hatari iliyokuwa inamkabili.

Mtu anayefikiria ni bora kwake kubakia katika dunia hii kufaidi starehe za dunia bila kujaribu kuifikia nirvana ni sawa kabisa na mtu yule aliyekataa kusaidiwa kuepuka hatari iliyokuwepo katika maisha yake ili ale asali..

(03) END

****